**JI. NO. 01**

# CHUO KIKUU TEOFILO KISANJI

S.L.P: 1104
MBEYA
TANZANIA
Simu: +255 (0)25 2502682
Simu: +255 696 592 252
Nukushi: +255 25 2503721
***Barua Pepe:*** info@teku.ac.tz
***Tovuti: www.teku.ac.tz***

*"Mafunzo Kwa Maisha Bora"*

**KITENGO CHA ELIMU ANUAI (CEP)**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KOZI ZA ASTASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

**Kumb: Na: TEKU/ASTAHAHADA/2026/2027/01**

**KWA: ……**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA ASTASHAHADA KOZI YA …….. (NGAZI YA 4) KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027.**

Makamu Mkuu wa Chuo, anapenda kukupongeza na kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya astashahada kwa kozi tajwa hapo juu katika **Chuo Kikuu Teofilo Kisanji – kilichopo Block T, Mbeya.** Mafunzo haya ni kwa mwaka mmoja (1) tu.

Chuo kitafunguliwa tarehe **25 Septemba, 2026 na usajili utaanza tarehe 25 Septemba mpaka tarehe 2 Oktoba 2026. Kuanzia tarehe 5 mpaka 9 Oktoba, 2026 Chuo kitaendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo na umahiri wanachuo katika fani za komputa, lugha na kanuni bora za maisha.**

Ili kukamilisha usajili na kupokelewa chuoni, unatakiwa kuleta vitu vifuatavyo:-

1. Vyeti halisi vya elimu ya kidato cha nne.
2. Picha za ***"Passport size"*** mbili zilizoandikwa kwa nyuma jina lako na kozi uliyo dahiliwa.
3. Cheti halisi cha kuzaliwa.
4. Barua ya maelezo kutoka kwa mdhamini wako; hii ni kwa wale wanaodhaminiwa tu.(taasisi, mashirika n.k)
5. Fomu ya afya iliyojazwa na daktari kutoka hospitali inayotambulika na serikali, (Medical examination form). Ambayo imeambatishwa katika barua hii ya maelekezo kabla ya kuja Chuoni.
6. Kompyuta mpakato/ Simu Janja

***MUHIMU: Hairuhusiwi kuleta au kuwasilisha taarifa zisizo sahihi.***

**Mambo Muhimu ya kuzingatia**

i. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Chuo Kikuu Teofilo Kisanji kwa maelezo ya utangulizi na usajili kuanzia tarehe 25 Septemba 2026.

ii. Mwanafunzi atasajiliwa kwa majina kama yalivyo kwenye cheti chake cha kidato cha nne.

iii. Mwanafunzi ataruhusiwa kuahirisha masomo kwa sababu maalumu, kama vile ugonjwa (vyeti vya daktari viambatanishwe), matatizo ya kifamilia pamoja na shida za ufadhili. utahitajika kuandika barua kwa Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma na kulipia kiasi cha shilingi Elfu Thelathini tu (30,000/=). Mwanafunzi ataruhusiwa kuahirisha masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja.

iv. Mwanafunzi apatapo changamoto yoyote, kuhitaji maulizo au ufafanuzi wowote, anashauriwa kuwasiliana na ofisi ya Mkuu wa Idara, Mshauri wa wanafunzi, au Msajili.

v. Uwapo chuoni mawasiliano yote yaonyeshe namba ya usajili na kozi unayosoma.

## UTARATIBU WA MALIPO

**kwa wanafunzi wa kozi mbalimbali za astashahada (NTA LEVEL 4)**

Kila mwanafunzi atapaswa kulipa Jumla ya shilingi milioni moja, laki tatu na mia mbili tu (1,300,200) kwa mwaka mzima na endapo atataka kulipa kwa awamu nne,gharama za kila awamu zimeainishwa kwenye majedwali kama ifuatavyo:

***Jedwali Namba 1: Jumla ya malipo kwa mwaka.***

| GHARAMA ZA MOJA KWA MOJA | KIASI |
|---|---|
| Usajili | 40,000.00 |
| Uthibitisho wa NACTVET | 20,000.00 |
| Udhibiti ubora TCU | 20,000.00 |
| Ada | 700,000.00 |
| Fedha ya mtihani | 100,000.00 |
| Fedha ya tahadhari (Hazirejeshwi) | 50,000.00 |
| Kitambulisho | 10,000.00 |
| Mafunzo kwa vitendo | 100,000.00 |
| Mchango wa maendeleo ya TEKU | 80,000.00 |
| Mahafali | 50,000.00 |
| Cheti cha matokeo | 30,200.00 |
| Mfuko wa Elimu Anuai | 100,000.00 |
| **JUMLA** | **1,300,200.00** |

***Malipo yafuatayo mwanafunzi aje nayo Chuoni, utaratibu wa malipo utatolewa Chuoni***

| | |
|---|---|
| Malipo ya serikali ya wanafunzi (TEKUSO) | 15,000.00 |
| Bima ya Afya (NHIF) | 50,400.00 |

**MUHIMU: Mwanafunzi anaruhusiwa kulipa kwa muhula au kwa mwaka mzima. Ili mwanafunzi asajiliwe ni lazima aje na fedha ya bima ya afya (NHIF).**

### 1. MALIPO YA AWAMU YA KWANZA

**Jedwali Namba 2. Usajili utafanyika baada ya kulipa kiasi cha laki nne na elfu hamsini na tano tu (455,000/) TEKUSO na NHIF, malipo ambayo yatahitajika kulipwa Mwezi Septemba, 2026.**

| GHARAMA ZA MOJA KWA MOJA | KIASI |
|---|---|
| Usajili | 40,000.00 |
| Ada | 175,000.00 |

| | |
|---|---|
| Uthibitisho wa NACTVET | 20,000.00 |
| Fedha ya tahadhari (hazirejeshwi) | 50,000.00 |
| Kitambulisho | 10,000.00 |
| Mfuko wa maendeleo ya TEKU | 40,000.00 |
| Udhibiti ubora wa TCU | 20,000.00 |
| Usimamizi wa mafunzo kwa vitendo | 50,000.00 |
| Mfuko wa Elimu Anuai | 50,000.00 |
| **JUMLA** | **455,000.00** |

***Malipo yafuatayo mwanafunzi aje nayo Chuoni, utaratibu wa malipo utatolewa Chuoni***

| | |
|---|---|
| Malipo ya serikali ya wanachuo (TEKUSO) | 15,000.00 |
| Bima ya Afya (NHIF) | 50,400.00 |

## 2. MALIPO YA AWAMU YA PILI

Mwanafunzi ataruhusiwa kuendelea na masomo endapo atakuwa amelipa ada na michango kama ilivyoainishwa hapo juu kwenye jedwali namba 2 pamoja na majedwali yafuatayo hapa chini:

**Jedwali namba 3. Mwanafunzi atahitajika kulipa kiasi cha laki mbili na elfu sitini na tano tu *(265,000) mpaka kufikia mwisho wa mwezi January, 2027)***

| GHARAMA ZA MOJA KWA MOJA | KIASI |
|---|---|
| Ada | 175,000.00 |
| Fedha ya mtihani | 50,000.00 |
| Mfuko wa maendeleo ya TEKU | 40,000.00 |
| **JUMLA** | **265,000.00** |

## 3. MALIPO YA AWAMU YA TATU

Awamu hii ya malipo hulipwa baada ya kufunguliwa chuo kwa muhula wa pili.

**Jedwali namba 4** Mwanafunzi atahitajika kulipa kiasi cha shilingi laki tatu na elfu ishirini na tano tu ( 325,000) kufikia mwisho wa mwezi wa Machi 2027

| GHARAMA ZA MOJA KWA MOJA | KIASI |
|---|---|
| Ada | 175,000.00 |
| Mafunzo kwa Vitendo | 50,000.00 |
| Fedha ya Mahafali | 50,000.00 |
| Mfuko wa Elimu Anuai | **50,000.00** |
| **JUMLA** | **325,000.00** |

## 4. MALIPO YA AWAMU YA NNE

*Awamu hii mwanafunzi atatakiwa kulipa kiasi cha laki mbili elfu hamsini na tano na miambili tu( **255,200)** kufikia mwisho wa mwezi **Mei, 2027***

**Jedwali Namba 5.**

| GHARAMA ZA MOJA KWA MOJA | KIASI |
|---|---|

| | |
|---|---|
| Ada | 175,000.00 |
| Cheti cha Matokeo | 30,000.00 |
| Fedha ya mtihani | 50,000.00 |
| **JUMLA** | **255,200.00** |

## 1. MFUMO WA MALIPO

Malipo yote yapitie kwenye akaunti rasmi za chuo kama zilivyoainishwa kama ifuatavyo:-

| Na. | JINA LA BENKI | NAMBA YA MALIPO (CONTROL NUMBER) | JINA LA AKAUNTI |
|---|---|---|---|
| **1** | **CRDB** | Tumia namba ya malipo utakayoomba kwa malipo yote ya **Ada**, **Michango mingine** na **Hostel**.<br><br>**Ili kupata namba ya malipo (Control number), piga simu namba: 0763509350/0749445079** | **TEOFILO KISANJI UNIVERSITY** |

**MUHIMU:** Baraza la Chuo lina haki ya kupitia na kufanya marejeo ya ada na michango mingine wakati wowote litakapohitajika kufanya hivyo.

Aidha, Mwanafunzi anakumbushwa kuwasilisha risiti ya malipo ya benki ofisi ya uhasibu **katika kipindi kisicho zidi siku tano(5),** ili upate risiti ya uthibitisho ya chuo baada ya kufanya malipo benki.

**HOSTELI**

**Malipo ya Hostel ni laki tatu tu (300,000) kwa mwaka mzima na inalipwa kwa awamu moja tu.**

**ZINGATIA:** Kwa mwanafunzi anayetarajia kukaa kwenye Hostel za Chuo, anatakiwa kufanya mawasiliano ya kuweka nafasi mapema; na ili kupata namba ya malipo tumia namba ya simu **0763509350/0743324305**. Usifanye malipo ya Hostel bila kuwasiliana na kujiridhisha uwepo wa nafasi.

## 2. GHARAMA ZISIZO ZA MOJA KWA MOJA

**Gharama za mahitaji hapa chini mzazi au mlezi atatakiwa kumpatia mwanafunzi kuja nazo:-**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Fedha ya serikali ya wanafunzi (TEKUSO) | 15,000.00 |
| 2 | Gharama ya bima ya afya (NHIF) | 50,400.00 |
| 3 | Fedha za chakula na kujikimu mwanafunzi awapo chuoni | |

**Tunakutakia ustawi mwema uwapo Chuo Kikuu Teofilo Kisanji….**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TEOFILO KISANJI UNIVERSITY-MBEYA**

*"Training for Better Life"*

**MEDICAL EXAMINATION FORM FOR STUDENTS**

**NAME OF THE INSTITUTION:** TEOFILO KISANJI UNIVERSITY

**PROGRAMME: …….. 2026/2027**

**PART A: STUDENT'S PARTICULARS**

STUDENT'S FULL NAME: **……**

DATE OF BIRTH: **……**

SEX: (Male/Female): **……** MARITAL STATUS: **……**

**PART B: STUDENT'S MEDICAL HISTORY**

Does the examinee have current history of any of the following? Indicate ***YES*** or ***NO***

Tuberculosis? .....

Epilepsy? .....

Sickle cell? ……

Asthmatic or with Allergic to something (*specify*)? ……..

Psychiatric? …… Vision impairment? ……..

Hearing disorder? …….

Physical disability? ……..

Any other significant medical condition/disorder? (*Please specify*) ……

## PART C: PHYSICAL EXAMINATION

Height (cm): ……. Weight (kg): …….. BP (mmHg): ……..

Any significant finding from systemic examinations (*please specify*):

……

……

……

……

## PART D: INVESTIGATIONS' FINDINGS

Please indicate any significant finding from the following Laboratory and Radiological tests

FBP:……... Urinalysis……..

Random Blood Sugar (*provide the results*): …… Blood group …….

Stool analysis: ……

Any other relevant investigation performed (*please give brief findings*):

……

……

……

## PART E: CONCLUSION

I have examined
Mr./Miss/Mrs…..... and consider that he/she is physically and mentally **fit/not fit** to be admitted to the University for studies.

**…….....** **……** **…….**

Name Signature Date

Qualification …… Title …….

Hospital's Name: ……...

(*Official hospital's stamp*)